# HOTUBA YA RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI, MHESHIMIWA DK. HUSSEIN ALI MWINYI, KATIKA HAFLA YA UZINDUZI WA VIWANJA VYA MICHEZO MATUMBAKU,

**TAREHE: 30 DISEMBA, 2023**

**Mheshimiwa Dkt. Saada Mkuya Salum;**
**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango,**

**Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo katika hafla hii,**

**Mheshimiwa Mhandisi Zena Ahmed Said;**
**Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi,**

**Dkt. Moh'd Said Moh'd (Dimwa)**
**Naibu Katibu Mkuu wa CCM, Zanzibar,**

**Mheshimiwa Idrissa Kitwana Mustafa;**
**Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja,**

**Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wa Wizara mliopo katika hafla hii,**

**Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama,**

**Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar,**

**Mkurugenzi Mwendeshaji Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar,**

**Viongozi mbali mbali wa Serikali na Vyama vya Siasa,**

**Ndugu Waandishi wa Habari,**

**Ndugu Wananchi,**

**Mabibi na Mabwana.**

**Assalam Aleikum.**

Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema kwa kutujaalia neema ya uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa kwa lengo la kushiriki hafla ya Uzinduzi wa Viwanja vya Michezo vya Kisasa katika eneo la Matumbaku hapa Miembeni Zanzibar.

Natoa shukrani zangu za dhati kwako Mheshimiwa Saada Mkuya Salum Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na wote walioshiriki kunialika niwe mgeni rasmi katika shughuli hii muhimu kwa maendeleo ya sekta ya michezo katika nchi yetu. Shukrani zangu maalum nazitoa kwenu viongozi nyote mliopo hapa, waalikwa na wananchi wote mliojitokeza kwa wingi katika kufanikisha shughuli hii. Nakushukuruni sana.

**Ndugu Wananchi**,

Tunakutana tena katika viwanja hivi kwa mara ya pili, ambapo siku ya tarehe 09 Januari,2023 tulikuwa hapa kwa ajili ya uwekaji wa jiwe la msingi baada ya kukamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa viwanja vitatu vya mpira wa miguu. Nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa Wizara ya Habari, vijana, Utamaduni na Michezo na Afisi ya Rais Fedha na Mipango pamoja na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kwa

kuyasimamia vyema maagizo niliyoyatoa siku ya uwekaji wa jiwe la msingi. Mtakumbuka niliagiza kuwa viwanja hivi ni lazima viwe vya kisasa vyenye muonekano mzuri kwa kujenga uzio na maegesho ya gari pamoja na kuweka sakafu maeneo yote. Pia nikaagiza kujengwa kwa viwanja vyengine kwa ajili ya michezo mingine ya mpira wa wavu (volleyball), mpira wa kikapu (basketball) na mpira wa kikapu (netball).

Katika hotuba yangu niliyoitoa siku hiyo niliahidi ya kuwa katika sherehe za miaka 60 ya Mapinduzi, tutarudi tena kufungua viwanja hivi baada ya kukamilika. Leo hii tupo hapa, nafarajika kuona kuwa kauli niliyoitoa siku ile na vyote nilivyoagiza vimezingatiwa na viwanja vimekamilika. Shukrani zangu ziende kwa watu wote waliofanikisha kukamilisha ujenzi wa viwanja hivi. Kwa hakika tuna haki ya kujivunia mafanikio makubwa ambayo nchi yetu imeyapata kwa ujenzi wa viwanja vya michezo vya kisasa ikizingatiwa kuwa juzi tu tumeufungua uwanja mpya wa Amaan uliofanyiwa matengenezo makubwa na hivi sasa umepata haiba mpya na kukidhi viwango vya michezo vya kimataifa.

**Ndugu wananchi**

Kwa lengo la kuimarisha sekta ya michezo, Serikali ya Awamu ya Nane imeamua kufanya jitihada maalum za kuimarisha miundombinu ya michezo ili kukuza vipaji vya vijana katika fani zote za michezo. Ndiyo maana tumekuja na utaratibu huu mpya wa kujenga viwanja vya michezo vya kisasa na tumekuwa tukishajiisha wawekezaji mbalimbali

kujenga viwanja vya michezo tofauti katika eneo moja (Sports Complex) kama hiki tunachokizindua leo hapa Matumbaku. Kuanzia sasa, lengo letu ni kuwa na maeneo ya michezo yenye kujumuisha viwanja vya michezo mbali mbali kwa pamoja kama tulivyoanzisha kule Amani kwa kujenga eneo la zaidi ya michezo kumi (10) inayoweza kuchezwa Katika viwanja tafauti vilivyoko pale.

**Ndugu wananchi**

Haya yote tunayafanya ili kuhakisha kuwa azma ya Serikali ya kuendeleza michezo katika nyanja zote inatimia kwa kuweka miundombinu iliyo bora na imara na hivyo vijana kupata nafasi ya kuonyesha vipaji vyao. Pia hatua hii itaziwezesha taasisi zinazohusika na michezo kuibua vipaji hivyo na kuvitumia katika kuitangaza nchi yetu kimichezo katika anga za kitaifa na Kimataifa. Aidha, kama inavyojulikana kuwa michezo nayo ni ajira, hivyo Serikali ya Awamu ya Nane inatilia mkazo ujenzi wa viwanja vya michezo mbalimbali ili kutanua wigo wa ajira kutokana na michezo.

Soko la ajira zinazotokana na michezo linakua kila kukicha na kufungua mipaka hadi kufikia katika maeneo ya mbali ya dunia. Tunaona wanamichezo wanaotoka katika nchi moja kwenda nchi nyengine kucheza michezo ya aina tofauti na kulipwa fedha nyingi. Niwaombe vijana watumie vizuri fursa za uwepo wa viwanja hivi kwa kuonyesha vipaji vyao ili waweze kujitengenezea ajira, iwe hapahapa Zanzibar au

hata nje ya Zanzibar. Pia, michezo ikitumika vizuri itakuwa ni moja kati ya namna ya kuitangaza Zanzibar na kukuza utalii ambao kwa kiasi kikubwa unachangia mapato ya nchi na kukuza uchumi wake.

**Ndugu wananchi,**

Nigusie mambo mawili ambayo kama tukiyafanyia kazi vizuri tutafungua milango kwa vijana wetu wa kizanzibari kupata fursa ya kuonyesha vipaji vyao na hatimae kupata nafasi ya kucheza michezo ya kulipwa Kimataifa. Jambo la kwanza ni hatua ambayo Tanzania imefikia kimichezo na hasa mpira wa miguu. Kupitia timu zetu kubwa za Yanga na Simba, katika michezo ya klabu bingwa na Shirikisho barani Afrika na kupelekea hata ufunguzi wa mashindano ya ligi ya Afrika kufanyika Tanzania na kuhudhuriwa na Rais wa FIFA na Rais wa CAF. Jambo hili ni mafanikio makubwa na linafungua milango kwa mpira wa Tanzania na Zanzibar na pia linachochea hamu ya wawekezaji kuwekeza katika mchezo wa mpira wa miguu na kuvutia ufadhili mkubwa. Jambo la pili ni nafasi ambayo Tanzania imeipata ya kushirikiana na Kenya na Uganda katika kuandaa mashindano ya AFCON ya mwaka 2027.

Ni wazi kuwa Serikali yetu ina dhamira na mipango madhubuti ya kuona kuwa Zanzibar inatajwa katika nyanja za Kimataifa za michezo. Lengo letu ni kuona na sisi tunapata nafasi ya kushiriki katika mashindano tofauti au kupata fursa ya kualika wageni mbalimbali mashuhuri kuja kujionea hatua ambazo Serikali inachukua katika kuweka miundo mbinu muhimu na mizuri ili kuendeleza vipaji vya vijana katika michezo.

**Ndugu wananchi,**

Nachukua fursa hii kuupongeza kwa dhati Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kwa juhudi mlizozifanya hadi leo hii tukaweza kuzindua viwanja hivi vya michezo katika eneo hili la Matumbaku. Nichukue fursa hii pia kujibu maombi ya wananchi wa Malindi ambao wameomba kupatiwa nafasi ya kutumia viwanja hivi baada ya viwanja vyao kutumika kwa ajili ya uwekezaji wa jengo la maegesho ya gari na kituo cha kisasa cha mabasi. Niwatoe hofu ndugu zangu wa Malindi, kwani moja ya dhamira ya ujenzi wa viwanja hivi ni kuwa mbadala wa maeneo yaliyofanyiwa uwekezaji. Lakini niwaombe Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuweka utaratibu mzuri ambao utahakiksha kuwa kila alie na haki ya kutumia viwanja hivi anapata nafasi hiyo. Aidha, Wizara ya Habari nawataka wasimamie vizuri matumizi yake ili ubora wake udumu kwa muda mrefu.

**Ndugu Wananchi,**

Kabla ya sijamaliza hotuba yangu, natoa shukrani zangu maalumu kwa uongozi wa JKU kwa kazi nzuri waliyoifanya. Natoa wito kwa wananchi wote washiriki kuunga mkono juhudi za Serikali na kuwa pamoja na wanamichezo katika kuutunza uwanja huu. Kwa mara nyengine, natoa shukurani kwako Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango na uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa kunialika kuja kushirikiana na wananchi wenzangu katika sherehe hizi za uzinduzi rasmi wa viwanja hivi vya michezo vya Matumbaku.

Kadhalika nawashukuru watu wote walioshiriki katika maandalizi ya shughuli hii. Pia natoa shukrani kwa viongozi wetu wa dini kwa kutuombea dua, wasanii wa sarakasi na utenzi kwa kutupatia burdani na waandishi wa habari kwa kuwapa taarifa wananchi wenzetu kuhusiana na tukio hili la maendeleo. Shukrani maalum kwa viongozi na wananchi wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Wilaya ya Mjini na Majimbo ya jirani kwa kujitokeza kwa wingi katika hafla hii ambayo ni katika shamra shamra za maadhimisho ya miaka 60 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. Tumuombe Mwenyezi Mungu aizidishie nchi yetu amani, umoja na mshikamano na atujaalie sote kila la kheri na mafanikio Katika kuuaga mwaka 2023 na kuukaribisha mwaka mpya 2024.

**Baada ya kusema hayo, sasa napenda kutamka kuwa viwanja vya Michezo vya Matumbaku vimefunguliwa rasmi.**

**Asanteni kwa Kunisikiliza.**